10

OFISIYAMTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

## OKTOBA, 2023

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA OKTOBA, 2023

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawiliya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 199 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Oktoba, 2023 ambapo waathirika walikuwa 199. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 78.9, wanawake asilimia 16.1 na wanaume asilimia 5.0. Miongoni mwa watoto, wasichana walikuwa 119 (asilimia 75.8) na wavulana walikuwa 38 (asilimia 24.2).

**Kielelezo 1.1: Asilimia ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Oktoba 2023**



Idadi ya Matukio ya Kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 89, ambapo waathirika 74 walikuwa wasichana na 15 walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 22 ambapo waathirika 21 walikuwa wavulana na mmoja alikuwa mwanamme. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni 13 ambapo wasichana walikuwa 11 na mawili (2) walikuwa wanawake. Matukio ya kutorosha ni 10 wote walikuwa wasichana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu ni 22 ambapo waathirika saba(7) ni wanawake,11 walikuwa wasichana na waathirika wanne (4) walikuwa wavulana. Matukio ya shambulio yalikuwa 43 ambapo waathirika 13 walikuwa wasichana, 13 walikuwa wavulana, nane (8) walikuwa wanawake na tisa (9) walikuwa wanaume.

**Kielelezo 1.2 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Oktoba, 2023**




Wilaya ya Mjini na Magharibi “B” zimeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 52) sawa na asilimia 26.1 kwa kila wilaya, ikifuatia wilaya ya Magahribi “A” ambapo yameripotiwa matukio 37 (asilimia 18.6). Wilaya ya Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio matatu (3) sawa na asilimia 1.5 kwa kila wilaya ukilinganisha na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Oktoba, 2023**







Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 26.8 kufikia matukio 199 mwezi wa Oktoba, 2023 kutoka matukio 157 kwa mwezi wa Septemba, 2023. Ambapo matukio ya Kubaka, Kulawiti na Kunajisi, Kuingilia kinyume na maumbile na shambulio yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Septemba 2023.

Wilaya ya Mjini na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 52) kwa kila wilaya kwa mwezi wa Oktoba, 2023 ambapo wilaya ya Magharibi "A" iliripotiwa kuongoza zaidi kwa mwezi wa Septemba, 2023 (matukio 41).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Septemba, 2023 na Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 |
| Kaskazini 'A' | 8 | 12 | 1 | 7 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 | 5 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 11 | 4 | 8 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 |
| Kati | 6 | 5 | 2 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 7 | 7 | 5 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 32 | 52 | 10 | 22 | 2 | 6 | 1 | 2 | 0 | 2 | 4 | 2 | 15 | 18 |
| Magharibi 'A' | 41 | 37 | 19 | 17 | 3 | 3 | 1 | 2 | 5 | 1 | 2 | 4 | 11 | 10 |
| Magharibi 'B' | 29 | 52 | 9 | 19 | 4 | 7 | 2 | 6 | 1 | 2 | 4 | 3 | 9 | 15 |
| Wete | 7 | 9 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 3 | 2 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 8 | 4 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **157** | **199** | **59** | **89** | **15** | **22** | **6** | **13** | **11** | **10** | **24** | **22** | **42** | **43** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 21.3. Jumla ya matukio yaliyoripotiwa kwa mwezi Oktoba, 2023 yalikuwa 199 na mwezi wa Oktoba, 2022 yaliripotiwa matukio 164. Matukio yote yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Oktoba, 2023 isipokuwa matukio ya Kulawiti na Kunajisi. Wilaya ya Mjini na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Oktoba, 2023 (matukio 52) kwa kila wilaya ambapo Wilaya ya Mjini iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Oktoba, 2022 (matukio 47).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Oktoba, 2022 na Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 | Okt 2022 | Okt 2023 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 12 | 3 | 7 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 11 | 2 | 8 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kati | 15 | 5 | 10 | 3 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 7 | 3 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 47 | 52 | 22 | 22 | 8 | 6 | 0 | 2 | 0 | 2 | 3 | 2 | 14 | 18 |
| Magharibi 'A' | 35 | 37 | 18 | 17 | 3 | 3 | 1 | 2 | 0 | 1 | 4 | 4 | 9 | 10 |
| Magharibi 'B' | 36 | 52 | 16 | 19 | 7 | 7 | 1 | 6 | 1 | 2 | 1 | 3 | 10 | 15 |
| Wete | 4 | 9 | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 8 | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 10 | 3 | 8 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **164** | **199** | **88** | **89** | **24** | **22** | **4** | **13** | **5** | **10** | **10** | **22** | **33** | **43** |

Miongoni mwa watoto 157 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 74, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 21, Kuingilia kinyume na maumbile ni wasichana 11, Kutorosha walikuwa wasichana 10, shambulio la aibu ni 15 kati yao wasichana walikuwa 11 na wavulana wanne (4) na shambulio walikuwa 26 kati yao wasichana walikuwa 13 na wavulana walikuwa 13.

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 5 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 39 | 18 | 6 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 5 | 5 |
| Magharibi 'A' | 29 | 15 | 2 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 3 | 3 |
| Magharibi 'B' | 44 | 17 | 7 | 6 | 2 | 0 | 2 | 0 | 5 | 5 |
| Wete | 8 | 2 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 7 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **157** | **74** | **21** | **11** | **10** | **0** | **11** | **4** | **13** | **13** |

Miongoni mwa wanawake 32 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 15, kuingilia kinyume na maumbile ni wanawake wawili (2), shambulio la aibu walikuwa wanawake saba (7) na shambulio walikuwa wanawake wanane (8).

**Jadweli 1.4a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 9 | 4 | 1 | 0 | 0 | 4 |
| Magharibi 'A' | 5 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| Magharibi 'B' | 5 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **32** | **15** | **2** | **0** | **7** | **8** |

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Magharibi 'A' | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **10** | **1** | **0** | **0** | **9** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 78) sawa na asilimia 49.7 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 38) sawa na asilimia 24.2. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 46) sawa na asilimia 62.2 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Oktoba, 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 6 | 4 | | | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 14 |
| 6-10 | | 6 | 10 | | | 6 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 1 | 27 |
| 11-14 | | 16 | 6 | | | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 4 | 6 | 38 |
| 15-17 | | 46 | 1 | | | 2 | 0 | 9 | 2 | 4 | 8 | 6 | 78 |
| **Jumla** | | **74** | **21** | | | **11** | **0** | **10** | **4** | **11** | **13** | **13** | **157** |




Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Oktoba, 2023 yamepungua wa asilimia 28.7 kufikia matukio 157 kwa mwezi wa Oktoba kutoka 122 kwa mwezi wa Septemba 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameongezeka kwa mwezi Oktoba, 2023 isipokuwa umri wa miaka 11-14 yameripotiwa kupungua kidogo kwa asilimia 0.03 kufikia waathirika 38 kutoka waathirika 39 kwa mwezi wa Septemba 2023.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Septemba 2023 na Oktoba 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 |
| 0- 5 | 6 | 6 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 4 | 0 | 0 | 14 | 14 |
| 06 -10 | 8 | 6 | 9 | 10 | 0 | 6 | 0 | 0 | 7 | 3 | 1 | 2 | 25 | 27 |
| 11-14 | 17 | 16 | 4 | 6 | 5 | 3 | 2 | 1 | 0 | 2 | 11 | 10 | 39 | 38 |
| 15-17 | 21 | 46 | 0 | 1 | 0 | 2 | 9 | 9 | 3 | 6 | 11 | 14 | 44 | 78 |
| **Jumla** | **52** | **74** | **15** | **21** | **5** | **11** | **11** | **10** | **16** | **15** | **23** | **26** | **122** | **157** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Oktoba, 2023 yameongezeka wa asilimia 12.1 kufikia matukio 157 kwa mwezi wa Oktoba, 2023 kutoka matukio 140 kwa mwezi wa Oktoba 2022. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameongezeka kwa mwezi Oktoba, 2023 isipokuwa umri wa miaka 6-14 yameripotiwa kupungua kwa mwezi wa Oktoba ya mwaka 2022.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Mwezi Oktoba, 2022 na Oktoba, 2023**

| Jumla | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 |
| 0-5 | 3 | 6 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 5 | 14 |
| 06-10 | 9 | 6 | 11 | 10 | 3 | 6 | 0 | 0 | 2 | 3 | 7 | 2 | 32 | 27 |
| 11-14 | 24 | 16 | 9 | 6 | 1 | 3 | 0 | 1 | 4 | 2 | 9 | 10 | 47 | 38 |
| 15-17 | 42 | 46 | 2 | 1 | 0 | 2 | 5 | 9 | 0 | 6 | 7 | 14 | 56 | 78 |
| **Jumla** | **78** | **74** | **24** | **21** | **4** | **11** | **5** | **10** | **6** | **15** | **23** | **26** | **140** | **157** |

Matukio mengi zaidi yanaonesha kutokea nyumbani kwa mtuhumiwa (matukio 70) sawa na asilimia 35.2 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Oktoba, 2023**




Matukio 139 kati ya matukio 199 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 69.9, matukio 57 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 28.6 na matukio matatu (3) lipo Mahakamani sawa na asilimia 1.5.

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Oktoba, 2023**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | M'mme | M'mke | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Zilizoachiwa Huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizochini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | W'chana | W'vulana | | | | | | |
| Kubaka | 89 | [redacted] | 15 | 74 | [redacted] | 2 | 0 | 0 | 0 | 25 | 62 |
| Kulawiti | 22 | 1 | [redacted] | [redacted] | 21 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 15 |
| Kuingiliwa kinyume na Maumbile | 13 | [redacted] | 2 | 11 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 8 |
| Kutorosha | 10 | 0 | 0 | 10 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 6 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 22 | 0 | 7 | 11 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 18 |
| Shambulio | 43 | 9 | 8 | 13 | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 30 |
| **Jumla** | **199** | **10** | **32** | **119** | **38** | **3** | **0** | **0** | **0** | **57** | **139** |

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | M'mme | M'ke | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Zilizoachwa Huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizochini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | W'chana | W'vulana | | | | | | |
| Kubaka | 89 | | 15 | 74 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 25 | 62 |
| Kulawiti | 22 | 1 | | | 21 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 15 |
| Kuingiliwa kinyume na Maumbile | 13 | | 2 | 11 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 8 |
| Kutorosha | 10 | 0 | 0 | 10 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 6 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 22 | 0 | 7 | 11 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 18 |
| Shambulio | 43 | 9 | 8 | 13 | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 30 |
| **Jumla** | **199** | **10** | **32** | **119** | **38** | **3** | **0** | **0** | **0** | **57** | **139** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Oktoba 2023 walikuwa 199 kati yao, 139 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 69.8 na 60 walikuwa jirani sawa na asilimia 30.2.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Oktoba, 2023**



## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA OKTOBA 2023

Jumla ya mashauri 29 yamefunguliwa katika mahkama za Udhalilishaji kwa mwezi wa oktoba,2023, ambapo mkoa wa Mjini umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 14) sawa na asilimia 48.3 ukilinganisha na mikoa mengine.

**Kielelezo 2.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Oktoba, 2023**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika mahkama za udhalilishaji Zanzibar ni 29. Ambapo mashauri, matatu (3) yametolewa uamuzi na mashauri 26 bado yanaendelea.

**Jadweli 2.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Oktoba, 2023**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Zilizotolewa uamuzi | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Faini | |
| Kubaka | 13 | 1 | 1 | 11 |
| Kubaka mgonjwa wa akili | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kujaribu kubaka | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kulawiti | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kujaribu kulawiti | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 3 | 0 | 0 | 3 |
| Kutorosha | 3 | 0 | 0 | 3 |
| Shambulio la aibu | 5 | 1 | 0 | 4 |
| **Jumla** | **29** | **2** | **1** | **26** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji ni 28 ambapo washtakiwa 27 walikuwa wanaume na mmoja (1) alikuwa mwanamke. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 19-21(washtakiwa 14) sawa na asilimia 50.

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 29 ambapo waathirika watatu (3) walikuwa wavulana na waathirika 26 walikuwa ni wasichana na wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 10-14 (waathirika 17) sawa na asilimia 58.6.

**Jadweli 2.2: Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Oktoba, 2023**

| Umri wa Mshtakiwa | Jinsi za Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Jinsi za Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 15-18 | 4 | 0 | 0-4 | 0 | 1 |
| 19-21 | 13 | 1 | 5-9 | 0 | 2 |
| 22-25 | 6 | 0 | 10-14 | 3 | 14 |
| 26-29 | 1 | 0 | 15-19 | 0 | 8 |
| 30-33 | 1 | 0 | 20-24 | 0 | 1 |
| 34-37 | 1 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 0 | 0 | 30-34 | 0 | 0 |
| 42-45 | 0 | 0 | 42-45 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 46-49 | 0 | 0 |
| 50-53 | 1 | 0 | 50-53 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **27** | **1** | **Jumla** | **3** | **26** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 199 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Oktoba, 2023 ambapo waathirika walikuwa 199. Wilaya ya Mjini na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 52) sawa na asilimia 26.1 kwa kila wilaya. Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 26.8 kufikia matukio 199 mwezi wa Oktoba, 2023 kutoka matukio 157 kwa mwezi wa Septemba, 2023.

Matukio 139 kati ya matukio 199 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 69.9, matukio 57 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 28.6 na matukio matatu (3) lipo Mahakamani sawa na asilimia 1.5.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Oktoba, 2023**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 4 | [redacted] | 4 | [redacted] | 1 | 1 | 1 | [redacted] | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 1 | 8 | 6 | 4 | 10 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 27 | [redacted] | 27 | [redacted] | 7 | 7 | 6 | [redacted] | 6 | 9 | 0 | 9 | 5 | 2 | 7 | 8 | 6 | 14 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 11 | [redacted] | 11 | [redacted] | 1 | 1 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 13 | [redacted] | 13 | [redacted] | 5 | 5 | 3 | [redacted] | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 |
| Sehemu nyengine (Vichakani na kwengine) | 34 | [redacted] | 34 | [redacted] | 8 | 8 | 3 | [redacted] | 3 | 1 | 0 | 1 | 3 | 1 | 4 | 5 | 10 | 15 |
| **Jumla** | **89** | [redacted] | **89** | [redacted] | **22** | **22** | **13** | [redacted] | **13** | **10** | **0** | **10** | **18** | **4** | **22** | **21** | **22** | **43** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Septemba, 2023 na Oktoba, 2023**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 | Sept 2023 | Okt 2023 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 4 | 4 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 12 | 8 | 9 | 10 | 27 | 24 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 16 | 27 | 6 | 7 | 4 | 6 | 7 | 9 | 5 | 7 | 14 | 14 | 52 | 70 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 8 | 11 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 1 | 16 | 13 |
| Sehemu za kazi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 2 | 3 |
| Skuli/ Madrasa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Majumba mabovu | 11 | 13 | 3 | 5 | 1 | 3 | 2 | 0 | 2 | 2 | 1 | 1 | 20 | 24 |
| Sehemu nyengine (Vichakanina kwengine) | 18 | 34 | 3 | 8 | 1 | 3 | 2 | 1 | 4 | 4 | 11 | 15 | 39 | 65 |
| **Jumla** | **59** | **89** | **15** | **22** | **6** | **13** | **11** | **10** | **24** | **22** | **42** | **43** | **157** | **199** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Oktoba, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 12 | 7 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 11 | 8 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kati | 5 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 7 | 3 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 52 | 22 | 6 | 2 | 2 | 2 | 18 |
| Magharibi 'A' | 37 | 17 | 3 | 2 | 1 | 4 | 10 |
| Magharibi 'B' | 52 | 19 | 7 | 6 | 2 | 3 | 15 |
| Wete | 9 | 2 | 1 | 1 | 1 | 4 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 4 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 |
| Mkoani | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **199** | **89** | **22** | **13** | **10** | **22** | **43** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Septemba, 2023 na Oktoba, 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 | Septemba 2023 | Oktoba 2023 |
| Kubaka | 59 | 89 | 7 | 15 | 52 | 74 | [redacted] | | | |
| Kulawiti | 15 | 22 | [redacted] | | | | 15 | 21 | 0 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 13 | 1 | 2 | 5 | 11 | [redacted] | | | |
| Kutorosha | 11 | 10 | 0 | 0 | 11 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 24 | 22 | 8 | 7 | 14 | 11 | 2 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio | 42 | 43 | 12 | 8 | 11 | 13 | 12 | 13 | 7 | 9 |
| **Jumla** | **157** | **199** | **28** | **32** | **93** | **119** | **29** | **38** | **7** | **10** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Oktoba, 2022 na Oktoba, 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 | Oktoba 2022 | Oktoba 2023 |
| Kubaka | 88 | 89 | 10 | 15 | 78 | 74 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] |
| Kulawiti | 24 | 22 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] | 24 | 21 | 0 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | 13 | 0 | 2 | 4 | 11 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] |
| Kutorosha | 5 | 10 | 0 | 0 | 5 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 10 | 22 | 4 | 7 | 6 | 11 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio | 33 | 43 | 10 | 8 | 10 | 13 | 13 | 13 | 0 | 9 |
| **Jumla** | **164** | **199** | **24** | **32** | **103** | **119** | **37** | **38** | **0** | **10** |

**Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Oktoba, 2023**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajis | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 5 | 1 | 0 | 1 | 2 | 2 | 11 |
| 03:01 - 06:00 Mchana | 15 | 4 | 0 | 2 | 1 | 2 | 24 |
| 06:01 - 09:00 Jioni | 9 | 2 | 1 | 0 | 5 | 3 | 20 |
| 09:01 - 12:00 Jioni | 16 | 5 | 3 | 4 | 7 | 6 | 41 |
| 12:01 - 03:00 Usiku | 28 | 7 | 6 | 3 | 6 | 8 | 58 |
| 03:01 - 06:00 Usiku | 11 | 3 | 2 | 0 | 1 | 12 | 29 |
| 06:01 - 09:00 Usiku | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 8 | 14 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| **Jumla** | **89** | **22** | **13** | **10** | **22** | **43** | **199** |

**Jadweli 6.0: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa na Aina ya Makosa**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 13 | 0 | 2 | 7 | 0 | 4 |
| Kubaka mgonjwa wa akili | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kujaribu kubaka | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kulawiti | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kujaribu kulawiti | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Shambulio la aibu | 5 | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **29** | **2** | **4** | **14** | **0** | **9** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa, Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanyabaadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosamengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

### Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136
MMP, Zanzibar.